BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# KITABU CHA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2015

# MAARIFA YA JAMII

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# KITABU CHA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2015

# MAARIFA YA JAMII

Kimechapishwa na

Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2015

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

YALIYOMO ........................................................................................ iii
DIBAJI ............................................................................................. iv
1.0 UTANGULIZI ........................................................................1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA .....................2
2.1 Sehemu A: Uraia ...................................................................2
2.2 Sehemu B: Historia...............................................................24
2.3 sehemu C: Jiografia...............................................................51
3.0 UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI .. .........................................................................................71
4.0 HITIMISHO ..........................................................................72
5.0 MAPENDEKEZO ..................................................................73
Kiambatanisho A.........................................................................74
Kiambatisho B.............................................................................77

# DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Maarifa ya Jamii mwaka 2015 imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya mtihani huo. Majibu ya wanafunzi katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo wanafunzi waliweza kujifunza kwa ufasaha na yale ambayo hawakuweza kujifunza kwa ufasaha katika kipindi cha miaka saba ya Elimu ya Msingi.

Katika taarifa hii, mambo mbalimbali ambayo yamechangia baadhi ya watahiniwa kuweza au kushindwa kujibu maswali kwa usahihi yameainishwa. Aidha , Uchambuzi unaonesha kuwa yafuatayo yamechangia kuwafanya watahiniwa kushindwa kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi: Kushindwa kutambua matakwa ya swali; kuwa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali; kutokuwa na ufahamu kabisa wa baadhi ya mada; kushindwa kuoanisha mada husika na maisha yao ya kila siku; kutojibu kabisa baadhi ya maswali au kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo katika mtihani. Uchambuzi wa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati watahiniwa walipokuwa wanajibu maswali zimeainishwa. Aidha, ulinganifu wa ufaulu wa watahiniwa kwa mada kati ya mwaka 2014 na 2015 umefanyika kwa kulinganisha mada zilizoongezeka ufaulu na zile zilizopungua.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, Baraza la

Mitihani la Tanzania linaamini kuwa endapo taarifa hii itafanyiwa kazi ipasavyo, ujuzi na maarifa watakayoyapata wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi vitaongezeka na hatimaye kiwango cha ufaulu katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi nacho kitaongezeka.

Mwisho, Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukurani za dhati kwa Maafisa Mitihani na wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii. Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kwa ujumla ambayo yatasaidia katika kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa siku zijazo.



**Dkt. Charles E. Msonde**

**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Maarifa ya Jamii ulifanyika tarehe 10 mwezi Septemba mwaka 2015. Jumla ya watahiniwa **808,085** walisajiliwa kufanya mtihani huo. Kati ya watahiniwa waliosajiliwa watahiniwa **763,510** ndio waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii. Uchambuzi wa majibu ya mtihani wa somo la Maarifa ya Jamii unaonesha kuwa watahiniwa **472,939 (61.94%)** ndio waliofaulu mtihani huo.

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Maarifa ya Jamii kwa mwaka 2015 ulikuwa na jumla ya maswali 50 yaliyogawanywa katika sehemu kuu tatu: Sehemu A: Uraia, Sehemu B: Historia na Sehemu C: Jiografia. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu zote tatu. Aidha, watahiniwa walielekezwa kuchagua jibu sahihi na kisha kuweka kivuli katika herufi ya jibu hilo katika karatasi ya kujibia. Majibu ya watahiniwa yamefanyiwa uchambuzi kwa kubainisha idadi ya watahiniwa waliofanya swali husika, chaguzi walizofanya na sababu zinazoweza kuwa zilichangia kuwafanya wasichague/wachague jibu sahihi.

Taarifa hii imegawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu uchambuzi wa majibu ya somo la Uraia, sehemu ya pili inaainisha uchambuzi wa majibu ya mtihani kwa somo la Historia na sehemu ya tatu inawasilisha uchambuzi wa somo la Jiografia.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA

### 2.1 Sehemu A: Uraia

**Swali la 1:** Mwenyekiti wa kikao cha maendeleo katika Kata ni

A Diwani wa Kata

B Afisa Huduma za Ugani

C Afisa Maendeleo wa Kata

D Mratibu Elimu wa Kata

E Afisa Mtendaji wa Kata.

**Jedwali 2.1**: Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 445,573 | 19,795 | 104,306 | 33,175 | 158,390 | 2,296 |
| Asilimia ya watahiniwa | 58.36 | 2.59 | 13.66 | 4.34 | 20.74 | 0.30 |

Swali lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu Mwenyekiti wa kikao cha maendeleo katika Kata. Swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 2.1** kwani watahiniwa 445,573 (58.36%) waliweza kuchagua jibu sahihi A “Diwani wa Kata”. Hii inaashiria kuwa watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu wa kutosha wa mada husika. Kipotoshi E “Afisa Mtendaji wa Kata” kiliwavutia watahiniwa wengi (20.74%) kwa kuwa ndiye mtendaji mkuu wa shughuli mbalimbali katika Kata likiwemo suala la maendeleo hivyo, watahiniwa huenda walidhani kuwa Afisa Mtendaji wa kata atakuwa pia ni mwenyekiti wa kikao cha maendeleo ya Kata.

Watahiniwa wengine (13.66%) walichagua kipotoshi C “Afisa Maendeleo wa Kata”. Watahinwa hawa pengine walichagua kipotoshi hiki kwa kudhani kuwa kwa vile Afisa Maendeleo wa Kata ni Mkuu wa Idara ya maendeleo ya jamii na msimamizi wa maendeleo ya jamii katika kata husika anaweza pia kuwa Mwenyekiti wa kikao cha Maendeleo ya Kata.

Watahiniwa wachache walichagua vipotoshi vingine kwa mtawanyiko uliokaribiana kama ifuatavyo; kipotoshi D “Mratibu Elimu wa Kata” asilimia 4.34 na B “Afisa Huduma za Ugani” asilimia 2.59. Kuwepo kwa idadi kubwa ya watahiniwa walioshindwa kuchagua jibu sahihi kunaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa muundo wa uongozi wa serikali za mitaa na mgawanyo wa majukumu katika ngazi ya Kata.

**Swali la 2:** Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa kwa pamoja zipo chini ya

A Bunge la Tanzania
B Serikali za Mitaa
C Serikali Kuu
D Wabunge wa kuchaguliwa
E Chama Tawala.

**Jedwali 2.2**: Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 149,411 | 267,353 | 252,389 | 41,253 | 50,336 | 2,793 |
| Asilimia ya watahiniwa | 19.57 | 35.02 | 33.06 | 5.4 | 6.59 | 0.37 |

Swali lilipima ufahamu wa watahiniwa kuhusu mada ya Serikali za Mitaa. Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kubainisha Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa kwa pamoja zipo chini ya chombo gani kati ya machaguo matano yaliyotolewa. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 267,353 tu sawa na asilimia 35.02 waliweza kuchagua jibu sahihi B “Serikali za Mitaa” kama ilivyoainishwa katika **Jedwali na. 2.2**. Watahiniwa hao waliweza kufahamu muundo wa Serikali za Mitaa. Kipotoshi C “Serikali Kuu” kiliwavutia watahiniwa wengi (33.06 %) ingawa hakikuwa sahihi. Pia kipotoshi A “Bunge la Tanzania “ kiliwavutia watahiniwa 149,411 sawa na asilimia 19.57. Vipotoshi vingine vilikuwa na mtawanyiko unaokaribiana kama ifuatavyo; D “Wabunge wa kuchaguliwa” asilimia 5.4 na E “Chama Tawala” asilimia 6.59. Kuwepo kwa idadi kubwa ya watahiniwa (64.99%) walioshindwa kuchagua jibu sahihi kunaashiria kuwa watahiniwa wengi hawana ufahamu wa kutosha wa muundo wa serikali za mitaa na hivyo kushindwa kutofautisha muundo wa Serikali za Mitaa na Serikali Kuu.

**Swali la 3:** Jukumu la kutunga sheria ndogondogo katika Halmashauri ya Wilaya ni la

A Mkuu wa Wilaya

B Afisa Sheria na Usalama wa Wilaya

C Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri

D Baraza la Madiwani

E Wabunge wa Wilaya husika.

**Jedwali 2.3**: Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 16,3952 | 100,892 | 109,822 | 283,338 | 101,341 | 4,190 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 21.47 | 13.21 | 14.38 | 37.11 | 13.27 | 0.55 |

Swali lilitoka katika mada ya Serikali za Mitaa ambapo watahiniwa walitakiwa kubainisha mamlaka yenye jukumu la kutunga sheria ndogondogo katika Halmashauri ya Wilaya. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na ufaulu hafifu kwani watahiniwa 283,338 sawa na asilimia 37.11 waliweza kuchagua jibu sahihi D “Baraza la Madiwani”.

Jumla ya watahiniwa 163,952 sawa na asilimia 21.47 walichagua kipotoshi A “Mkuu wa Wilaya”. Kipotoshi hiki kiliwavutia watahiniwa pengine kwa sababu ya kuwepo neno “wilaya” katika shina la swali hivyo kuhusisha moja kwa moja na neno “Mkuu wa Wilaya”. Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakuwa na ufahamu kuwa Mkuu wa Wilaya hayupo katika muundo wa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya. Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi vingine katika mtawanyiko unaokaribiana kama ifuatavyo; B “Afisa Sheria na Usalama wa Wilaya” (13.21%), C “Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri” (14.38%) na E “Wabunge wa Wilaya husika” (13.27%).

Kuwepo kwa idadi kubwa ya watahiniwa (62.88%) walioshindwa kubaini jibu sahihi kunaashiria kuwa watahiniwa

hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya Majukumu ya Baraza la Madiwani katika Halmashauri ya Wilaya.

**Swali 4:** Kati ya alama zifuatazo ni ipi inapatikana katika bendera ya Rais?

A Nyundo.

B Pembe za Ndovu.

C Nembo ya Taifa.

D Ramani ya Tanzania.


E Ramani ya Afrika.

Swali liliwataka watahiniwa kubaini alama inayopatikana katika bendera ya Rais kutoka katika machaguo matano yaliyotolewa. Swali lilikuwa na ufaulu mzuri kuliko maswali mengine kwani asilimia 73.99 ya watahiniwa waliweza kubaini jibu sahihi ambalo ni C "Nembo ya Taifa." Hii inadhihirisha kuwa asilimia kubwa ya watahiniwa walikuwa na ufahamu mzuri wa mada ya Alama za Taifa.

Aidha, watahiniwa 198,613 walishindwa kubaini jibu sahihi na kukosa kwa uwiano unaokaribiana kwa kuchagua vipotoshi vilivyosalia ambavyo ni A "Nyundo" (8.98%),B "Pembe za ndovu" (8.33%), D "Ramani ya Tanzania" (6.02%) na E "Ramani ya Afrika" (2.29%). Watahiniwa waliochagua A "Nyundo" hawakuelewa kuwa nyundo si alama katika Bendera ya Rais. Aidha, watahiniwa walichagua B "Pembe za Ndovu." hawakuwa na ufahamu kuwa Pembe za Ndovu ni miongoni mwa alama katika Nembo ya Taifa.

Watahiniwa waliochagua D “Ramani ya Tanzania” hawakujua kuwa hakuna ramani katika bendera ya Rais. Watahiniwa waliochagua E “Ramani ya Afrika” hawakujua kuwa ramani ya Afrika haina uhusiano na Bendera ya Rais wa Tanzania. Kwa ujumla kushindwa kwa watahiniwa hawa kubaini jibu sahihi ni kiashiria kuwa walikuwa na uelewa mdogo wa mada ya Alama za Taifa hususan Bendera ya Rais.

**Kielelezo 2.1**: Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo




***Kielelezo 2.1:*** *Kinaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 73.99 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi.*

**Swali la 5:** Katika Nembo ya Taifa alama inayowakilisha maliasili ya taifa ni

A mlima Kilimanjaro

B mkuki

C karafuu

D pembe za ndovu

E mawimbi ya bahari.

**Jedwali 2.4**: Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 141,366 | 68,191 | 81,996 | 411,032 | 57,069 | 3,881 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 18.51 | 8.93 | 10.74 | 53.83 | 7.47 | 0.50 |

Swali lililenga kupima ufahamu wa watahiniwa kuhusu alama inayowakilisha maliasili katika Nembo ya Taifa. Watahiniwa walitarajiwa kuwa na ufahamu wa kutosha kwani Nembo ya Taifa ipo katika sehemu nyingi ikiwemo katika nyaraka za serikali, ofisi za serikali, fedha na katika Bendera ya Rais. Fedha na nyaraka nyingi za serikali zinaweza kupatikana kwa urahisi katika mazingira ya shule ama nyumbani. Nembo ya Taifa ni kielelezo cha uwezo, umoja, uhuru na nguvu za taifa. Hata hivyo, kama inavyooneshwa katika **Jedwali 2.4,** ni watahiniwa 411,032 tu sawa na asilimia 53.83 waliweza kuchagua jibu sahihi D "pembe za ndovu".

Watahiniwa 348,622 (45.65%) walikosa swali hili kwa kuchagua vipotoshi kwa mtawanyiko ufuatao; Kipotoshi A "mlima Kilimanjaro" asilimia 18.51, B "mkuki" asilimia 8.93, C "karafuu" asilimia 10.74 na E" mawimbi ya bahari" asilimia 7.47. Mkuki, karafuu, mlima Kilimanjaro na mawimbi ya bahari zote ni alama katika Nembo ya Taifa ila haziwakilishi maliasili ya Taifa. Mlima Kilimanjaro unawakilisha mlima mrefu kuliko yote barani Afrika, mkuki ni kielezo cha silaha za kujihami na kujilinda dhidi ya maadui, karafuu ni kielelezo cha mazao ya biashara yanayolimwa Tanzania na mawimbi ya bahari inawakilisha Bahari ya Hindi, mito na maziwa yaliyopo

Tanzania. Hivyo, watahiniwa walikosa ufahamu kuhusu Nembo ya Taifa na uwakilishi wa kila alama katika nembo hiyo.

**Swali la 6:** Ni muhimu kwa wapiga kura wenye sifa kushiriki katika uchaguzi wa Rais na Wabunge kwa sababu

A ni njia ya amani ya kubadili uongozi wa nchi
B ni njia pekee ya kuimarisha utandawazi
C ni kanuni ya kuimarisha mshikamano
D ni kanuni ya mfumo wa vyama vingi
E ni njia pekee ya kuleta mabadiliko ya Katiba ya nchi.

**Jedwali 2.5**: Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 365,338 | 44,885 | 55,933 | 84,965 | 208,112 | 4,302 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 47.85 | 5.88 | 7.33 | 11.13 | 27.26 | 0.57 |

Swali lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusiana na umuhimu wa wapiga kura wenye sifa kushiriki katika uchaguzi wa Rais na Wabunge. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 2.5** ambapo jumla ya watahiniwa 365,338 (47.85%) walichagua A "ni njia ya amani ya kubadili uongozi wa nchi". Watahiniwa waliochagua jibu hili walikuwa na ufahamu kuhusu malengo mahsusi ya mchakato wa kidemokrasia katika kuchagua Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Watahiniwa walioshindwa kuchagua jibu sahihi walikuwa na mtawanyiko wa majibu kama ifuatavyo: Jumla ya watahiniwa 208,112 (27.26%) walichagua herufi E “ni njia pekee ya kuleta mabadiliko ya Katiba ya nchi”. Yawezekana watahiniwa hawa walivutiwa na jibu hili kutokana na mijadala ya mabadiliko ya katiba hivi karibuni katika Bunge la Katiba. Bunge hilo maalumu lilijumuisha pia wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, watahiniwa walihusisha dhana ya wananchi kuchagua wabunge na mjadala wa mabadiliko ya katiba jibu ambalo halikuwa sahihi. Watahiniwa 55,933 (7.33%) walichagua C “ni kanuni ya kuimarisha mshikamano”. Watahiniwa waliochagua jibu hili hawakuwa na ufahamu mzuri juu ya matakwa ya swali.

Watahiniwa 84,965 (11.13%) walichagua D “ni kanuni ya mfumo wa vyama vingi”. Ni ukweli kuwa Tanzania inafuata mfumo wa vyama vingi vya siasa ambao hutoa ushindani kwa wagombea wa nafasi ya Urais, Wabunge na Madiwani kutoka vyama mbalimbali vya siasa kushiriki katika uchaguzi kwa lengo la kupata ridhaa ya wananchi ili kuunda na kuongoza serikali. Watahiniwa waliochagua jibu hili walishindwa kuelewa kuwa swali lilihusu sababu ya wapiga kura kushiriki katika uchaguzi wa Rais na Wabunge na halikulenga kubainisha mfumo wa demokrasia unaofuatwa. Jumla ya watahiniwa 44,885 (5.88%) walichagua kipotoshi B “ni njia pekee ya kuimarisha utandawazi” jibu ambalo pia halikuwa sahihi kwani hakuna uhusiano kati ya wananchi kushiriki uchaguzi wa Rais na Wabunge na suala zima la utandawazi.

Watahiniwa hawa walionesha uelewa mdogo katika mada ya Ushindani wa Kidemokrasia katika siasa.

**Swali la 7:** Kuzingatia sheria, haki za binadamu, ukweli na uwazi, na uhuru wa vyombo vya habari ni misingi ya

A urasimu

B utawala wa sheria

C ujamaa wa kiafrika

D demokrasia ya uwakilishi

E utawala bora.

**Jedwali 2.6**: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 31,950 | 92,281 | 42,080 | 144,838 | 448,334 | 4,052 |
| Asilimia ya watahiniwa | 4.18 | 12.09 | 5.51 | 18.97 | 58.72 | 0.53 |

Swali lilitoka katika mada ya Misingi ya Demokrasia na lililenga kupima ufahamu wa watahiniwa kuhusu misingi ya utawala bora ambayo ni kuzingatia sheria, haki za binadamu, ukweli na uwazi, na uhuru wa vyombo vya habari. Kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.2.6** ufaulu wa watahiniwa ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 448,334 sawa na asilimia 58.72 waliweza kuchagua jibu sahihi E “utawala bora”. Watahiniwa waliochagua jibu hili walionesha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusiana na misingi ya utawala bora hivyo kutovutiwa na vipotoshi vingine. Jumla ya watahiniwa 144,838 (18.97%) walichagua D “demokrasia ya uwakilishi”

ambalo sio jibu sahihi. Watahiniwa hawa huenda walivutiwa na kipotoshi hiki kwa sababu ya uwepo wa neno ‘Demokrasia’ ambalo linajulikana kwa watahiniwa wengi, hivyo ilikuwa rahisi kwa watahiniwa kuvutiwa na kipotoshi hiki.

Watahiniwa 92,281 (12.09%) walichagua kipotoshi B “utawala wa sheria”. Watahiniwa hawa huenda walichagua kipotoshi hiki kutokana na kuwepo neno ‘sheria’ katika kiini cha swali hivyo kuhusisha neno ‘sheria’ na dhana ya utawala wa sheria ambao ni msingi wa sheria unaotamka kuwa watu wote na taasisi lazima wafuate sheria na kuwajibika kwa sheria inayotumika bila upendeleo na kutekelezwa.

Idadi ya watahiniwa 42,080 (5.51%) walichagua C “ujamaa wa kiafrika” wakati watahiniwa wengine 31,950 (4.18%) walichagua A “urasimu” ambayo yote hayakuwa majibu sahihi. Watahiniwa walioangukia katika kundi hili wanaonesha kuwa hawana ufahamu wa mada ndogo ya utawala bora.

**Swali la 8:** Ipi kati ya orodha zifuatazo inawakilisha makundi ya kutetea haki za wanawake Tanzania?

A UWT, TAWLA na TAMWA.

B TAMWA, TGNP na TAWLA.

C MEWATA, TGNP na TAWLA.

D UWT, TGNP na TAMWA.

E MEWATA, TGNP na UWT.


Swali la 8 lililenga kupima ufahamu wa watahiniwa kubaini makundi yanayotetea haki za wanawake Tanzania kati ya

makundi matano waliyopewa. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani ni watahiniwa 208,289 tu sawa na asilimia 27.28 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi B “TAMWA, TGNP na TAWLA” kama ilivyoainishwa katika **Kielelezo 2.2**. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa mzuri kuhusu makundi yanayotetea haki za wanawake Tanzania.

Kipotoshi A “UWT, TAWLA na TAMWA” kilichaguliwa na asilimia kubwa ya watahiniwa (43.36%). Watahiniwa waliochagua kipengele hiki huenda walivutiwa na neno “UWT” ambalo ni kifupi “Umoja wa Wanawake Tanzania”. Kimsingi UWT ni Umoja wa Wanawake ndani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) tu.

Vipotoshi vingine vilikuwa na mtawanyiko ufuatao: C “MEWATA, TGNP na TAWLA” asilimia 13.82, D “UWT, TGNP na TAMWA” asilimia 8.44 na E “MEWATA, TGNP na UWT” asilimia 6.41. Kuwepo kwa idadi kubwa ya watahiniwa (72.03%) walioshindwa kuchagua jibu sahihi kunaashira kuwa watahiniwa wengi hawana ufahamu wa kutosha kuhusu makundi yanayotetea haki za wanawake. Mbali na kuwepo kwenye Muhtasari, vitabu, magazeti na majarida mbali mbali, elimu kuhusu haki za wanawake imekuwa ikitolewa na asasi hizo kwa njia mbalimbali kama vile vyombo vya habari na mikutano.

**Kielelezo 2.2:** Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo




***Kielelezo 2.2.*** *kinaonesha kuwa ni watahiniwa wachache tu (27.28%) walioweza kubaini jibu sahihi.*

**Swali la 9**: Jukumu la kuwalinda raia wa Tanzania na mali zao lipo mikononi mwa

A Jeshi la Wananchi la Tanzania

B Idara ya Usalama wa Taifa

C Jeshi la Magereza

D Jeshi la Mgambo

E Jeshi la Polisi.

**Jadwali Na 2.7:** Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 256,723 | 72,813 | 29,699 | 35,693 | 364,271 | 4,336 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 33.62 | 9.54 | 3.89 | 4.67 | 47.71 | 0.57 |

Swali lilitoka katika mada ya Ulinzi na Usalama wa Taifa. Swali lilipima uelewa wa watahiniwa katika kubainisha jeshi

lenye jukumu la kuwalinda raia na mali zao. Kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.2.7** swali lilikuwa na ufaulu wa wastani ambapo watahiniwa 364,271 (47.71%) waliweza kubaini jibu sahihi kwa kuchagua E “Jeshi la Polisi”. Watahiniwa walioweza kuchagua jibu hili walikuwa na uelewa mzuri kuhusu jeshi lenye jukumu la msingi la kulinda raia na mali zao.

Jumla ya watahiniwa 399,264 (52.29%) walikosa swali hili kwa kuchagua majibu yasiyo sahihi katika mtawanyiko ufuatao: watahiniwa 256,723 (33.62%) A “Jeshi la Wananchi la Tanzania”, watahiniwa 72,813 (9.54%) B “Idara ya Usalama wa Taifa”, watahiniwa 29,699 (3.89%) C “Jeshi la Magereza” na watahiniwa 35,693 (4.67%) “Jeshi la Mgambo”. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivi hawakuwa na uelewa kwamba japo kuna majeshi mengi, kila jeshi lina jukumu lake la msingi na jukumu la kulinda raia na mali zao lipo mikononi mwa Jeshi la Polisi.

**Swali la 10:** Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) lilianzishwa mwaka

A 1961

B 1962

C 1964

D 1963

E 1965.

**Jadwali Na 2.8** Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 111,365 | 110,725 | 322,851 | 95,824 | 117,191 | 5,579 |
| Asilimia ya watahiniwa | 14.59 | 14.5 | 42.28 | 12.55 | 15.35 | 0.73 |

Swali lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kubainisha mwaka ambao Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) lilianzishwa. Kama ilivyooneshwa katika **jedwali 2.8** Watahiniwa 322,851 (42.28%) waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni C "1964." Hii inamaanisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa sahihi juu ya kuanzishwa kwa JWTZ. Watahiniwa 117,191 (15.35%) walichagua herufi E " 1965". Hili halikuwa jibu sahihi. Aidha, watahiniwa hao huenda walivutiwa na kipotoshi hiki kutokana na kila mwaka uliowekwa katika vipengele vingine kuwa na tukio kubwa katika historia ya nchi na hivyo kudhani kuwa mwaka 1965 ni jibu sahihi miongoni mwa miaka iliyoorodheshwa.

Watahiniwa 111,365 (14.59%) walichagua kipotoshi A "1961". mwaka ambao Tanganyika ilipata uhuru wake kutoka mikononi mwa wakoloni. Watahiniwa 110,725 (14.5%) walivutiwa na kipotoshi B "1962" pengine kwa vile mwaka huo Tanganyika ilikuwa Jamhuri hivyo ingewezekana pia jeshi la ulinzi lilianzishwa mwaka huo. Watahiniwa 95,824 (12.55%) walichagua D "1963" ambalo halikuwa sahihi. Watahiniwa hawa walishindwa kubaini kuwa mwaka 1963 lilianzishwa

Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na siyo mwaka wa kuanzishwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

**Swali la 11**: Ni muhimu kwa Tanzania kuendeleza lugha ya Kiswahili kwa sababu ni lugha

A inayozungumzwa na watu wengi Afrika ya Mashariki
B ya mawasiliano katika Umoja wa Mataifa
C ya kufundishia shuleni
D inayowaunganisha watanzania
E ya mawasiliano katika Bunge la Tanzania.

**Jadwali Na 2.9** Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadiya watahiniwa | 191,540 | 74,322 | 55,257 | 404,491 | 33,988 | 3,937 |
| Asilimia ya watahiniwa | 25.09 | 9.73 | 7.24 | 52.98 | 4.45 | 0.52 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha umuhimu wa Tanzania kuendeleza Lugha ya Kiswahili kati ya machaguo matano ya majibu waliyopewa. Kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.2.9** ufaulu wa watahiniwa ulikuwa wa wastani ambapo watahiniwa 404,491 (52.98%) waliweza kubaini jibu sahihi kwa kuchagua D "Lugha inayowaunganisha watanzania". Watahiniwa waliochagua jibu hili walionesha kuwa na ufahamu mzuri wa umuhimu wa kuendeleza Lugha ya Kiswahili hivyo hawakuvutiwa na vipotoshi ambavyo vilikuwa na mapungufu kadhaa.

Watahiniwa wengine waliangukia katika machaguo ambayo hayakuwa majibu sahihi kama ifuatavyo: Watahiniwa 191,540 (25.09%) walichagua A "lugha inayozungumzwa na watu wengi Afrika ya Mashariki". Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakuwa na ufahamu kuwa kuzungumzwa na watu wengi kwa lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki sio sababu kuu ya Tanzania kuiendeleza Lugha ya Kiswahili.

Watahiniwa 74,322 (9.73%) walichagua B "lugha ya mawasiliano katika Umoja wa Mataifa" ambalo siyo jibu sahihi. Aidha, kipotoshi C "lugha ya kufundishia shuleni" kilichaguliwa na watahiniwa 55,257 (7.24%). Watahiniwa hawa huenda walivutiwa na kipotoshi hiki kwa sababu Kiswahili ni lugha ya kufundishia katika shule nyingi za msingi kuanzia darasa la I hadi la VII lakini walishindwa kufahamu kuwa Kiswahili si lugha pekee ya kufundishia kwani Kiingireza pia hutumika kufundishia katika shule zote za sekondari na baadhi ya shule za msingi. Watahiniwa 33,988 (4.45%) walichagua E "lugha ya mawasiliano katika Bunge la Tanzania" pengine walidhani kuwa kwa kuwa lugha hiyo hutumika Bungeni ndiyo maana kuna haja ya kuiendeleza jibu ambalo halikuwa sahihi pia.

**Swali la 12:** Zipo aina tatu za mipango ya uchumi ambayo ni mipango ya

A miaka kumi, kumi na tano na ishirini na tano
B Taifa, Mkoa na Wilaya
C kilimo, biashara na viwanda

D muda mrefu, dharura na muda mfupi

E muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.


Swali lililenga kupima ufahamu wa watahiniwa kuhusu aina tatu za mipango ya uchumi. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa hafifu kwani watahiniwa wachache tu 114,347 (14.98%) waliweza kubaini jibu sahihi E “muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu” kama ilivyoainishwa katika **Kielelezo 2.3**. Watahiniwa waliochagua jibu hili walionesha kuwa na uelewa mzuri wa mada ndogo ya Sera na Mipango ya Uchumi na hawakuvutiwa na machaguo mengine ambayo hayakuwa majibu sahihi.

Watahiniwa wengine walichagua machaguo mengine ambayo hayakuwa sahihi kama ifuatavyo: Watahiniwa 379,286 (49.67%) walichagua C “kilimo, biashara na viwanda”. Watahiniwa waliochagua jibu hili hawakuwa na ufahamu kuwa kilimo, biashara na viwanda si aina za mipango ya uchumi bali ni shughuli za kiuchumi zinazohusu uzalishaji mali.

Watahiniwa 147,169 (19.27%) walichagua B “Taifa, Mkoa na Wilaya”. Watahiniwa hawa hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuwa Taifa, Mkoa na Wilaya ni ngazi za usimamizi na utekelezaji wa mipango ya kiuchumi. Aidha, watahiniwa 70,739 (9.26%) waliochagua D “muda mrefu, dharura na muda mfupi”, hawakuelewa kuwa “dharura” haijumuishwi kwenye mipango ya kiuchumi. Watahiniwa hawa pengine walivutiwa na kuwepo kwa maneno “muda mrefu” na “muda mfupi” katika kipotoshi hicho lakini wakashindwa kufahamu

kuwa kuwepo kwa neno "dharura" kumefanya kipotoshi D kukosa maana iliyokusudiwa hivyo kutokuwa jibu sahihi. Watahiniwa 47,588 (6.23%) walichagua A "miaka kumi, kumi na tano na ishirini na tano". Majibu haya hayakuwa sahihi kwani hakuna mipango ya uchumi ya aina zilizotajwa katika kipotoshi hicho.

**Kielelezo 2.3:** Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo.




***Kielelezo 2.3** kinaonesha kuwa ni watahiniwa wachache sana (14.98%) waliweza kubaini jibu sahihi.*

**Swali la 13:** Moja ya athari mbaya ya utandawazi kwa Tanzania ni

A kuongezeka kwa idadi ya wageni nchini

B kumomonyoka kwa maadili katika jamii

C kuongezeka kwa uhasama baina ya vyama vya siasa

D kuongezeka kwa uhuru wa vyombo vya habari

E ongezeko la matumizi ya teknolojia ya habari.


Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kubainisha moja ya athari mbaya ya utandawazi kwa Tanzania. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyofanywa vizuri na watahiniwa walio wengi kwani jumla ya watahiniwa 491,521 sawa na asilimia 64.37 waliweza kubaini moja ya athari mbaya ya utandawazi kwa Tanzania kwa kuchagua herufi B “kumomonyoka kwa maadili katika jamii” kama ilivyoainishwa katika **Kielelezo 2.4.** Kuwepo kwa watahiniwa wengi walioweza kubaini jibu sahihi kunashiria kuwa watahiniwa walikuwa na uelewa mkubwa wa athari za utandawazi Tanzania.

Jumla ya watahiniwa 86,283 (11.3%) walichagua A “kuongezeka kwa idadi ya wageni nchini”. Licha ya ukweli kuwa utandawazi unaruhusu kuongezeka kwa muingiliano wa watu kutoka sehemu moja kwenda nyingine, watahiniwa hawa hawakuelewa kuwa kuongezeka tu kwa wageni hakuwezi kuwa na athari mbaya kwa Tanzania hivyo jibu hili halijitoshelezi kulinganisha na matakwa ya swali. Watahiniwa 89,576 sawa na asilimia 11.73 walichagua herufi C “kuongezeka kwa uhasama baina ya vyama vya siasa”. Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki walishindwa kubaini kuwa kwenye vyama vya siasa hakuna uhasama bali ushindani wa sera kwa ajili ya kupata ridhaa ya wananchi ili kuunda serikali hivyo kufanya kipotoshi hiki kutokuwa sahihi.

Aidha, watahiniwa 54,134 (7.09%) walichagua herufi E “ongezeko la matumizi ya teknolojia ya habari” wakati watahiniwa 37,717 (4.94%) walichagua D “kuongezeka kwa uhuru wa vyombo vya habari”. Watahiniwa waliochagua

vipotoshi hivi walikosa umakini katika kuchambua machaguo yaliyokuwa yametolewa ili kubaini jibu sahihi linalobeba dhana nzima ya athari mbaya ya utandawazi kwa Tanzania.

**Kielelezo 2.4**: Asilimia ya Watahiniwa katika kila Chaguo.




***Kielelezo 2.4** kinaonesha kuwa ni watahiniwa wengi (64.37%) waliweza kubaini jibu sahihi.*

**Swali la 14:** Utawala wa sheria maana yake ni

A wananchi kujichukulia sheria mkononi
B polisi kuadhibu wanaovunja sheria
C sheria kuchukua mkondo wake
D mahakama kukamata wanaovunja sheria
E mamlaka ya Mahakama kutunga sheria.

**Jadwali Na 2.10:** Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 104,210 | 73,272 | 401,822 | 91,838 | 87,305 | 5,088 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.65 | 9.6 | 52.63 | 12.03 | 11.43 | 0.67 |

Swali hili lilitoka mada ya Misingi ya Demokrasia na lilipima ufahamu wa watahiniwa kuhusiana na maana ya Utawala wa sheria. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani ambapo watahiniwa 401,822 (52.63%) waliweza kuchagua jibu sahihi C “sheria kuchukua mkondo wake”. Watahiniwa waliochagua jibu hili walionesha uelewa mkubwa kuhusu maana ya utawala wa sheria.

Watahiniwa 356,625 sawa na aslimia 46.71 walikosa katika mtawanyiko wa chaguzi zinazokaribiana (kati ya asilimia 9.6 hadi 13.65) kama ifuatavyo: Watahiniwa 104,210 (13.65%) walichagua A “wananchi kujichukulia sheria mkononi”. Watahiniwa waliochagua jibu hili hawakuwa na ufahamu kuwa kujichukulia sheria mkononi ni kinyume cha utawala wa sheria. Watahiniwa 91,838 (12.03%) walichagua D “mahakama kukamata wanaovunja sheria”. Watahiniwa hawa hawakufahamu kuwa kazi ya mahakama si kukamata wanaovunja sheria bali ni kusimamia sheria na kutoa hukumu kwa wale wanaopatwa na hatia kwa mujibu wa sheria. Watahiniwa 87,305 (11.43%) walichagua E “mamlaka ya Mahakama kutunga sheria”. Watahaniwa walikuwa na uelewa

mdogo kuhusu kazi za mahakama kuwa si kutunga sheria. Sheria kwa mujibu wa katiba zinatungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi ya mahakama ni kutafsiri sheria zilizotungwa na bunge. Kwa ujumla watahiniwa hawa walivutiwa na kuwepo kwa neno “sheria” katika swali na “mahakama” katika majibu yaliyopendekezwa hivyo kudhani kuwa yanahusiana na maana ya “utawala wa sheria”.


Watahiniwa wengine 73,272 (9.6%) walichagua kipotoshi B “polisi kuadhibu wanaovunja sheria” jibu ambalo halikuwa sahihi. Watahiniwa hawa hawakuwa na ufahamu sahihi kuhusu kazi ya Jeshi la polisi kuwa si kuwaadhibu wanaovunja sheria bali ni kuwakamata wanaotuhumiwa kuvunja sheria na kuwafikisha mahakamani. Kwa mujibu wa sheria mahakama ndicho chombo pekee chenye mamlaka ya kuthibitisha mtu aliyevunja sheria. Kwa ujumla, watahiniwa hawa walikosa ufahamu wa dhana ya utawala wa sheria na hivyo kujikuta wakivutiwa na vipotoshi hivyo.

## 2.2 Sehemu B: Historia

**Swali la 15:** Familia hujumuisha

A marafiki, watoto na ndugu
B baba, mama na watoto
C majirani, ndugu na watoto
D majirani, watoto na marafiki
E baba, mama na majirani.

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha watu ambao wanaunda familia. Swali hili lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyokuwa na ufaulu mzuri kwani watahiniwa wengi (90.59%) waliweza kuchagua jibu sahihi B “baba, mama na watoto” kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na.2.2.1.** Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya Familia Yetu pengine kwa sababu waliweza kuhawilisha maarifa kutoka katika familia zao. Aidha, asilimia 7.06 ya watahiniwa waliochagua A “marafiki, watoto na ndugu”, C “majirani, ndugu na watoto”, D “majirani, watoto na marafiki na E “baba, mama na majirani” walishindwa kuelewa kuwa marafiki na majirani siyo sehemu ya wanafamilia.




***Kielelezo Na.2.2.1** kinaonesha kuwa watahiniwa wengi walichagua jibu sahihi.*

**Swali 16:** Mahitaji ya lazima ya familia ni pamoja na

A chakula, malazi na magari

B chakula, mavazi na televisheni


C mavazi, malazi na chakula

D chakula, malazi na televisheni

E mavazi, chakula na magari.

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini mahitaji ya lazima ya familia. Kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na.2.2.2**, watahiniwa wengi (86.24%) walichagua jibu sahihi ambalo ni C “mavazi, malazi na chakula” Watahiniwa hawa walifahamu kuwa familia inahitaji chakula, malazi na mavazi ili iweze kuishi. Aidha, asilimia 13.44 ya watahiniwa waliochagua A “chakula, malazi na magari”, B “chakula, mavazi na televisheni”, D “chakula, malazi na televisheni” na E “mavazi, chakula na magari” walishindwa kuelewa kuwa magari na televisheni siyo mahitaji ya msingi katika familia. Uchaguzi wa vipotoshi hivi yawezekana umechangiwa na mtindo wa maisha wa sasa katika familia nyingi zenye uwezo wa kifedha ambapo magari na televisheni huchukuliwa kama mahitaji ya msingi hivyo kufanya watahiniwa kushindwa kutofautisha kati ya mahitaji ya msingi na mahitaji mengine.

**Kielelezo Na. 2.2.2:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.




**Kielelezo Na.2.2.2** *kinaonesha kuwa watahiniwa wengi walichagua jibu sahihi.*

**Swali la 17:** Binadamu wa kale alianza kilimo na ufugaji katika Zama za

A Kati za Mawe

B Mwisho za Mawe

C Mwanzo za Mawe


D Chuma

E Shaba.

Swali hili liliwataka watahiniwa kubaini Zama ambazo binadamu wa kale alianza kulima mazao na kufuga wanyama. Jibu sahihi lilikuwa B "Zama za Mwisho za Mawe"

ambalo lilichaguliwa na asilimia 44.1 ya watahiniwa kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na.2.2.3** Watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu wa kutosha wa hatua za maendeleo zilizokuwa zimefikiwa na binadamu katika kila Zama. Aidha, asilimia 27.57 ya watahiniwa waliochagua A "Zama za Kati za Mawe" na asilimia 8.79 ya watahiniwa waliochagua C "Zama za Mwanzo za Mawe" walishindwa kuelewa kuwa maendeleo makubwa yaliyokuwa yamefikiwa na binadamu katika vipindi hivi viwili ni ugunduzi wa moto pamoja na utengenezaji wa zana mbalimbali za mawe ambazo hazikuwa bora kuliko zile zilizotengenezwa enzi za Zama za Mwisho za Mawe. Aidha, asilimia 15.84 ya watahiniwa waliochagua D "Zama za Chuma" pengine walivutiwa na kipotoshi hiki kutokana na mchango wa chuma katika kumwezesha binadamu kuyatawala mazingira yake. Watahiniwa hawa walipaswa kuelewa kuwa binadamu alianza kilimo na ufugaji katika Zama za Mwisho za mawe baada ya kuanzisha makazi ya kudumu. Aidha, asilimia 3.19 ya watahiniwa walichagua kipotoshi E "Zama za Shaba" hawakuwa na uelewa kuhusu vipindi vya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kiteknolojia ambavyo binadamu alipitia.

**Kielelezo Na.2.2.3:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.





***Kielelezo Na.2.2.3*** *kinaonesha kuwa swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani.*

**Swali la 18:** Michoro ya mapangoni iliyoko Kondoa Irangi inasadikiwa kuchorwa katika Zama za

A Mwanzo za mawe
B Kati za mawe
C Mwisho za mawe
D Chuma
E Ugunduzi wa moto.

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini kipindi ambacho michoro ya mapangoni iliyoko Kondoa Irangi inasadikiwa kuchorwa. **Kielelezo Na.2.2.4** kinaonesha kuwa jibu sahihi C “mwisho za mawe” lilichaguliwa na watahiniwa wachache (21.68%) ambao walikuwa na uelewa wa hatua za maendeleo zilizokuwa zimefikiwa na binadamu katika vipindi

mbalimbali. Watahiniwa wengi (66.83%) walichagua vipotoshi A, B na D kwa sababu walishindwa kubaini maendeleo ya mwanadamu katika zama mbalimbali. Aidha, watahiniwa waliochagua E "ugunduzi wa moto" (10.95%) hawakuwa na uelewa wa kutosha wa neno "Zama" kwani ugunduzi wa moto hazikuwa "Zama" bali ni tukio la kihistoria lililotokea katika Zama za Kati za Mawe. Hii inaashiria kuwa watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha "Zama" na "matukio."




**Kielelezo Na. 2.2.4** *kinaonesha kuwa ni watahiniwa wachache tu waliweza kuchagua jibu sahihi.*

**Swali la 19:** Mkataba wa kufunga soko la watumwa la Zanzibar ulisainiwa mwaka

A 1822

B 1845

C 1885

D 1884

E 1873.

**Jedwali Na.2.2.1:** Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 82,387 | 103,651 | 120,362 | 96,922 | 355,740 | 4,473 |
| Asilimia ya watahiniwa | 10.79 | 13.58 | 15.76 | 12.69 | 46.6 | 0.59 |

Swali lilipima uelewa wa watahiniwa katika kubaini mwaka ambao mkataba wa kufunga soko la watumwa la Zanzibar ulisainiwa. Karibia nusu ya watahiniwa (46.6%) walichagua jibu sahihi E "1873" kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.2.2.1**. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mikataba mbalimbali iliyolenga kukomesha biashara ya utumwa hivyo ilikuwa rahisi kwao kubaini mkataba uliosababisha kufungwa kwa soko la watumwa. Hata hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi A "1822" (10.79%) na B "1845" (13.58%) walikuwa na uelewa juu ya mikataba iliyosainiwa kukomesha biashara ya utumwa lakini walishindwa kubaini mwaka ambao mkataba uliosababisha kufungwa kwa soko la watumwa Zanzibar ulisainiwa. Watahiniwa hawa walipaswa kuelewa kuwa mkataba uliosainiwa mwaka 1822 (Mkataba wa Moresby) ulilenga kumzuia Sultan Seyyid Said kusafirisha watumwa nje ya himaya yake ilhali mkataba wa mwaka 1845 (Hamerton) ulimkataza Sultan Seyyid Said kusafirisha watumwa nje ya Afrika Mashariki. Watahiniwa waliochagua vipotoshi C "1885" (15.76%) na D "1884" (12.69%) walishindwa kutofautisha kati ya Biashara ya Utumwa na Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika

kwani miaka hiyo ilihusu Mkutano wa kuligawa bara la Afrika miongoni mwa mataifa ya kibeberu. Watahiniwa hawa pengine walivutiwa na vipotoshi hivi kutokana na umaarufu wa Mkutano wa Berlin ulioitishwa 1884 – 1885. Aidha, watahiniwa 4,473 sawa na asilimia 0.59 baadhi hawakujibu kabisa swali hili na wengine walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 20:** Moja ya faida ya uhusiano wa kibiashara kati ya Tanganyika na jamii nyingine ilikuwa

A kukua kwa miji ya pwani ya Afrika Mashariki kama Kilwa na Lagos
B kukua kwa dola za Afrika Mashariki kama vile Buganda na Songhai
C kupatikana kwa bidhaa zilizokuwa hazizalishwi nchini
D kuingizwa kwa silaha Tanganyika
E kukomeshwa kwa biashara ya utumwa.

**Jedwali Na.2.2.2:** Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 146,801 | 99,103 | 347,117 | 39,260 | 125,785 | 54.69 |
| Asilimia ya watahiniwa | 19.23 | 12.98 | 45.46 | 5.14 | 16.5 | 0.71 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha moja ya faida ya uhusiano wa kibiashara kati ya Tanganyika na jamii nyingine. Kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.2.2.2**, karibia nusu ya watahiniwa (45.46%) walichagua jibu sahihi C “kupatikana

kwa bidhaa zilizokuwa hazizalishwi nchini". Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa kuwa sababu kubwa iliyofanya Tanganyika kujihusisha katika shughuli za biashara ilikuwa ni kupata bidhaa ambazo zilikuwa hazipatikani katika maeneo yao kutokana na sababu ya hali ya hewa na sababu za kijiografia. Hata hivyo, asilimia 32.21 ya watahiniwa waliochagua A "kukua kwa dola na miji ya pwani ya Afrika Mashariki kama Kilwa na Lagos" na B "kukua kwa dola za Afrika Mashariki kama vile Buganda na Songhai" walikuwa na ufahamu kuwa biashara kati ya jamii mbalimbali zilisababisha kukua kwa baadhi ya dola na miji lakini walishindwa kuelewa kuwa "Songhai" na "Lagos" hazikuwa miongoni mwa dola wala miji katika Afrika Mashariki. Aidha, asilimia 16.5 ya watahiniwa waolichagua kipotoshi E "kukomeshwa kwa biashara ya utumwa" walishindwa kuelewa kuwa kukomeshwa kwa biashara ya utumwa kulichochea kuingia kwa ukoloni katika Afrika wakati asilimia 5.14 ya watahiniwa waliochagua D "kuingizwa kwa silaha Tanganyika" walishindwa kuelewa kuwa silaha zilizoingizwa Tanganyika kwa kiasi kikubwa zilichochea mapigano kati ya jamiii moja na nyingine.

**Swali la 21:** Nani alikuwa gavana wa kwanza wa Kijerumani katika Tanganyika?

A Julius Von Soden

B Albert Von Rechenberg

C Herman Von Wissman

D Friedrich Von Schele

E Carl Peters.

**Jedwali Na.2.2.3:** Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 401,745 | 58,980 | 110,334 | 36,569 | 150,740 | 5,167 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 52.62 | 7.72 | 14.45 | 4.79 | 19.7 | 0.68 |

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini Gavana wa kwanza wa Kijerumani katika Tanganyika. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.2.2.3,** kwani asilimia 52.62 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi A "Julius Von Soden" ambaye alikuwa Gavana wa kwanza wa Kijerumani kuanzia mwaka 1891 hadi 1893. Watahiniwa waliochagua B "Albert Von Rechenberg", C "Herman Von Wissman" na D "Friedrich Von Schele" hawakuelewa kwamba hawa walikuwa ni magavana wa kijerumani katika Tanganyika waliofuata baada ya Julius Von Soden kama ifuatavyo; Friedrich Von Schele (1893-1895), Herman Von Wissman(1895-1896) na Albert Von Rechenberg (1906-1912). Aidha, kipotoshi E "Carl Peters" kiliwavutia asilimia 19.7 ya watahiniwa huenda kwa sababu Carl Peters ni maarufu miongoni mwa wanahistoria kutokana na mchango wake katika kuingiza ukoloni wa Kijerumani nchini Tanganyika kupitia mikataba ya ulaghai aliyosaini na watawala wa jadi.

**Swali la 22:** Mwanzilishi wa mfumo wa utawala wa mlango wa nyuma katika Afrika alikuwa


A Horace Byatt

B Fredrick Lugard

C Richard Turnbull

D Donald Cameroon

E Edward Twinning.




**Kielelezo Na.2.2.5** *kinaonesha kuwa zaidi ya robo ya watahiniwa walichagua jibu sahihi*.

Swali hili liliwataka watahiniwa kubaini mwanzilishi wa mfumo wa utawala wa mlango wa nyuma katika Afrika. Ni asilimia 26.08 tu ya watahiniwa waliweza kujibu swali hili kwa usahihi kwa kuchagua B “Fredrick Lugard” kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na.2.2.5.** Watahiniwa hawa walidhihirisha ufahamu mzuri wa Utawala wa Mlango wa Nyuma wa Waingereza ambao ulishirikisha watawala wa jadi katika uongozi wake katika kutawala makoloni. Watahiniwa waliochagua vipotoshi A (17.7%), C (19.98%), D (20.78%) na E (15.2%) walihusianisha utawala wa Kiingereza katika Tanganyika na mfumo wa utawala wa mlango wa nyuma pengine kwa kuwa mfumo huu ulitumika katika kuitawala

Tanganyika chini ya magavana hawa lakini walishindwa kuelewa kuwa mfumo huu ulianzishwa kwa mara ya kwanza na Fredrick Lugard nchini Nigeria.

**Swali la 23:** Mkutano wa Berlin wa mwaka 1884 -1885 uliitishwa na

A Carl Peters

B Johann Krapf


C Henry Stanley

D David Livingstone

E Otto Von Bismarck.

Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kubaini kiongozi aliyeitisha Mkutano wa Berlin wa mwaka 1884 - 1885. Ufaulu katika swali hili, kama inavyoonesha kwenye **Kielelezo Na.2.2.6**, ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 400,547 sawa na asilimia 52.5 waliweza kuchagua jibu sahihi E "Otto Von Bismarck." Aidha, watahiniwa 140,700 sawa na asilimia 18.43 walichagua kiposhi A "Carl Peters." Kipotoshi hiki kilichaguliwa na idadi kubwa ya watahiniwa pengine kutokana na umaarufu wa Carl Peters ambaye alisaini mikataba mingi ya ulaghai na watawala wa jadi katika Tanganyika. Asilimia 28.43 ya watahiniwa waliochagua vipotoshi B "Johann Krapf", C "Henry Stanley" na D "David Livingstone" walishindwa kuelewa kwamba Johann Krapf, Henry Stanley na David Livingstone walikuwa ni wapelelezi maarufu waliyochangia kwa kiwango kikubwa kutawaliwa kwa Afrika lakini hawakuitisha mkutano wa Berlin.

**Kielelezo Na.2.2.6:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.




**Kielelezo Na.2.2.6** *kinaonesha kuwa zaidi ya nusu ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi.*

**Swali la 24:** Tanganyika na Zanzibar ziliungana mwaka

A 1964

B 1961

C 1962


D 1977

E 1963.

Swali hili lilipima uelewa wa watahiniwa katika kubaini mwaka ambao Tanganyika na Zanzibar ziliungana. Hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na ufaulu mzuri kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na.2.2.7**, kwani asilimia

65.44 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi A "1964". Ufaulu mzuri katika swali hili pengine ulichangiwa na umaarufu wa siku ya muungano ambayo mbali ya kuwa inafundishwa darasani, husheherekewa kila mwaka na hutangazwa sana kwenye vyombo vya habari. Watahiniwa waliochagua kipotoshi B "1961" (13.69%) walishindwa kutofautisha kati ya mwaka ambao Tanganyika ilipata uhuru na mwaka ambao Tanganyika na Zanzibar ziliungana. Kwa upande mwingine, asilimia 20.37 ya watahiniwa waliochagua vipotoshi C"1962", D "1977" na E"1963" walifahamu kwamba miaka hiyo ilihusu matukio mbalimbali ya kihistoria yaliyotokea katika Tanganyika/Tanzania lakini walishindwa kuelewa kuwa Tanganyika ilikuwa jamhuri mwaka 1962, mwaka 1963 Zanzibar ilipata uhuru wa bendera ilihali mwaka 1977 chama cha TANU (Tanganyika African Union) na ASP (Afro Shiraz Party) viliungana na kuzaa CCM (Chama Cha Mapinduzi). Uwepo wa asilimia 34.06 ya watahiniwa waliochagua majibu yasiyo sahihi kunaonesha kuwa zaidi ya theluthi ya watahiniwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha wa miaka ya matukio ya kihistoria licha ya ukweli kwamba matukio hayo hutangazwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama redio, magazeti na televisheni na husheherekewa kila mwaka.

**Kielelezo Na.2.2.7**: Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.




**Kielelezo Na.2.2.7** *kinaonesha kuwa watahiniwa wengi waliweza kuchagua jibu sahihi.*

**Swali la 25:** Azimio la Arusha lililenga

A kuboresha maisha ya matajiri vijijini

B kutaifisha mali za wazungu na kuzigawa kwa maskini

C kupunguza tofauti ya kipato miongoni mwa raia

D kukomesha ubaguzi wa rangi nchini


E kudumisha amani katika nchi jirani.

Swali hili liliwataka watahiniwa kubaini mojawapo ya misingi ya Azimio la Arusha. Ni asilimia 27.22 tu ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi C “kupunguza tofauti ya kipato miongoni mwa raia” kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na.2.2.8**. Watahiniwa hawa walidhihirisha kuwa na uelewa

wa kutosha kuhusu mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika Afrika huru. Kipotoshi D “kukomesha ubaguzi wa rangi” kilivutia watahiniwa wengi (38.16%) pengine kwa sababu walihusianisha harakati za ukombozi kusini mwa Afrika zilizolenga kukomesha ubaguzi wa rangi na Azimio la Arusha.

Aidha, asilimia 33.94 ya watahiniwa waliochagua vipotoshi A “kuboresha maisha ya matajiri”, B “kutaifisha mali za wazungu na kuzigawa kwa maskini” na E “kudumisha amani katika nchi jirani” walikosa ufahamu wa kutosha kuhusu Azimio la Arusha na malengo yake. Ufaulu huu mdogo (27.22%) katika swali hili unaashiria kuwa watahiniwa hawakuielewa vyema mada ya Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru.

**Kielelezo Na.2.2.8:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.




**Kielelezo Na.2.2.8** *kinaonesha kuwa watahiniwa wengi walishindwa kuchagua jibu sahihi.*

**Swali la 26:** Ipi kati ya nchi zifuatazo ilipata uhuru kwa njia ya vita?

A Zimbabwe.

B Tanganyika.

C Ghana.

D Malawi.

E Zambia.

**Jedwali Na.2.2.4:** Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 322,731 | 142,774 | 144,163 | 87,977 | 60,927 | 4,963 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 42.27 | 18.7 | 18.88 | 11.52 | 7.98 | 0.65 |

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini nchi ambayo ilipata uhuru kwa njia ya vita. Swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwani ni asilimia 42.27 tu ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi A “Zimbabwe” kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.2.2.4.** Watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu mada ya Jitihada za Kupigania Uhuru katika Afrika hivyo waliweza kubaini utaratibu wa kudai uhuru uliotumiwa na nchi mbalimbali katika bara la Afrika kama vile njia ya amani na njia ya vita.

Hata hivyo, asilimia 57.08 ya watahiniwa waliochagua vipotoshi B “Tanganyika”, C “Ghana”, D “Malawi” na E “Zambia” hawakuwa na uelewa juu ya njia zilizotumiwa na kila nchi kudai uhuru wake. Watahiniwa hawa walipaswa kuelewa kwamba nchi nyingi zilizopata uhuru kwa njia ya vita

zilikuwa na walowezi wengi. Baadhi ya nchi hizo ni Zimbabwe, Angola na Msumbiji. Aidha, Tanganyika, Ghana, Malawi na Zambia zilipata uhuru kwa njia ya amani kwani hazikuwa na walowezi wengi.

**Swali la 27:** Lengo mojawapo la kuanzishwa kwa UNO lilikuwa

A kuunganisha nchi zinazoendelea

B kuleta umoja wa Waafrika

C kupinga ukoloni mamboleo


D kudumisha amani

E kutengeneza silaha bora.

Swali hili lilipima ufahamu wa watahiniwa katika kubaini lengo mojawapo la kuanzishwa kwa UNO. Kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na.2.2.9**, jibu sahihi ni D “kudumisha amani” lililochaguliwa na watahiniwa 291,295 sawa na asilimia 38.15. Watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu wa kutosha juu ya malengo ya kuanzishwa kwa UNO. Kipotoshi B “kuleta umoja wa Waafrika” kilivutia watahiniwa wengi (30.14%) pengine kwa sababu watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha kati ya malengo ya Umoja wa Mataifa na yale ya Umoja wa Nchi huru za Kiafrika (OAU). Watahiniwa hawa walipaswa kuelewa kwamba chombo kilichoanzishwa kwa lengo la kuleta umoja wa Waafrika ni Umoja wa Afrika (AU) na sio Umoja wa Mataifa (UNO). Hata hivyo, asilimia 31.1 ya watahiniwa waliochagua A “kuunganisha nchi zinazoendelea”, C “kupinga ukoloni mamboleo” na E “kutengeneza silaha bora”

hawakuwa na ufahamu juu ya malengo ya kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa.

**Kielelezo Na.2.2.9:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.




**Kielelezo Na.2.2.9** *kinaonesha kuwa ni watahiniwa wachache tu waliweza kuchagua jibu sahihi.*

**Swali la 28:** Mji wa Katanga ulikuwa maarufu kwa utoaji wa

A dhahabu
B shaba
C ulanga
D almasi
E petroli.

**Jedwali Na. 2.2.5:** Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 135,271 | 251,398 | 172,640 | 89,375 | 108,891 | 5,960 |
| Asilimia ya watahiniwa | 17.72 | 32.93 | 22.61 | 11.71 | 14.3 | 0.71 |

Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha aina ya madini yalioufanya mji wa Katanga kuwa maarufu. Kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.2.2.5** jumla ya watahiniwa 251,398 sawa na asilimia 32.93 waliweza kuchagua jibu sahihi B "Shaba". Watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu kuhusu sababu kuu za uhusiano wa jamii za Kitanzania na jamii nyingine za Kiafrika hivyo, ilikuwa rahisi kwao kutambua kuwa shaba ilikuwa bidhaa maarufu ambayo watu wa Katanga waliitumia kubadilishana na bidhaa kutoka jamii zingine. Hata hivyo, kuwepo kwa idadi kubwa ya watahiniwa (66.34%) waliokosa swali hili kwa kuchagua vipotoshi A "dhahabu", C "ulanga", D "almasi" na E "petroli" kunadhihirisha kuwa watahiniwa hawa walishindwa kuelewa maeneo ambayo yalikuwa maarufu kwa uzalishaji wa aina mbalimbali za bidhaa kabla ya ukoloni.

**Swali la 29:** Kabla ya utawala wa Waingereza, Zanzibar ilikuwa ikitawaliwa na

A Kansela


B Gavana

C Malkia

D Sultani

E Mtemi.

Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha kiongozi aliyekuwa akiitawala Zanzibar kabla ya utawala wa Waingereza. Kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na.2.2.10**, watahiniwa wengi (60.27%) waliweza kuchagua jibu sahihi D “ Sultani” kwa sababu walikuwa na ufahamu wa kutosha juu ya tawala mbalimbali za kikoloni Zanzibar. Jumla ya watahiniwa 129,489 (16.96%) walivutiwa na kipotoshi B “Gavana” pengine kwa sababu walishindwa kutambua kwamba kabla ya utawala wa Waingereza, Zanzibar ilikuwa ikitawaliwa na Sultani. Asilimia 13 ya watahiniwa waliochagua A “Kansela” na C “Malkia” walishindwa kutambua kwamba Kansela na Malkia walikuwa ni viongozi wa juu wa Kijerumani na Kiingereza kwa mfuatano huo, ambao kwa mfumo wa utawala wa kikoloni walikuwa wakipewa taarifa na magavana kuhusu hali na maendeleo ya makoloni. Aidha, asilimia 9.23 ya watahiniwa waliochagua E “Mtemi” walishindwa kutambua kwamba huyu alikuwa ni kiongozi mkuu katika jamii za wanyamwezi na wasukuma.




**Kielelezo Na.2.2.10** *kinaonesha kuwa zaidi ya nusu ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi.*

**Swali la 30:** Kampuni ya biashara ya Kijerumani ilishindwa kuitawala Tanganyika kutokana na

A kuja kwa Wareno

B upinzani kutoka kwa Waafrika

C miundombinu bora iliyokuwepo

D mikataba ya ulaghai

E kuondoka kwa Waingereza.

**Jedwali Na.2.2.6:** Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 100,176 | 333,634 | 125,065 | 145,625 | 53,385 | 5,650 |
| Asilimia ya watahiniwa | 13.12 | 43.7 | 16.38 | 19.07 | 6.99 | 0.74 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha sababu iliyosababisha Kampuni ya biashara ya Kijerumani kushindwa kuitawala Tanganyika. Kama inavyooonekana katika **Jedwali Na.2.2.6**, jibu sahihi lilikuwa B “upinzani kutoka kwa Waafrika” na lilichaguliwa na watahiniwa 333,634 sawa na asilimia 43.7. Watahiniwa hawa walitambua mchango wa upinzani kutoka kwa Waafrika ambao ulipelekea kumalizika kwa utawala wa kampuni ya biashara ya Kijerumani.

Aidha, asilimia 13.12 ya watahiniwa waliochagua kipotoshi A “kuja kwa Wareno” walishindwa kutambua kuwa Wareno waling’olewa Afrika ya Mashariki katika karne ya 17 ilhali kampuni ya biashara ya Kijerumani iliingia Tanganyika katika karne ya 19. Aidha, asilimia 19.07 ya watahiniwa waliochagua kipotoshi D “mikataba ya ulaghai” walishindwa kubaini kuwa mikataba ya ulaghai iliyosainiwa na Carl Peters iliwawezesha Wajerumani kuanzisha utawala wao katika Tanganyika na sio kudhoofisha utawala wa kampuni hii.

Hata hivyo, asilimia 23.37 ya watahiniwa waliochagua vipotoshi C “miundombinu bora iliyokuwepo” na E “kuondoka kwa Waingereza” walishindwa kuelewa kuwa miondombinu bora ina mchango chanya katika kuendeleza ustawi wa kampuni yoyote wakati kuondoka kwa Waingereza halikuwa jibu sahihi kwani kampuni hii haikuwa na uhusiano wowote na Waingereza.

**Swali la 31:** Utafutaji wa njia ya kwenda India ulifadhiliwa na

A Vasco Da Gama

B Bartholomew Diaz


C Cecil Rhodes

D Mfalme Henry

E Henry Stanley.

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha jina la mtu aliyefadhili utafutaji wa njia ya kwenda India. Kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na.2.2.11**, ni watahiniwa 123,572 tu sawa na asilimia 16.18 walichagua jibu sahihi D “Mfalme Henry”. Aidha, watahiniwa wengi (43.4%) walivutiwa na kipotoshi A “Vasco Da Gama”. Hii inaweza kuwa imesababishwa na umaarufu wa Vasco Da Gama ambaye alikuwa baharia na mpelelezi wa kwanza wa Kireno kufika India kupitia Rasi ya Tumaini Jema. Watahiniwa hawa walipaswa kuelewa kuwa safari zote za utafiti wa njia ya kwenda India katika karne ya 15 zilizofanywa na mabaharia na wapelelezi wa Kireno kama vile Vasco Da Gama na Bartholomew Diaz zilifadhiliwa na Mfalme Henry. Vilevile asilimia 24.19 ya watahiniwa walichagua B “Bartholomew Diaz” walishindwa kutambua mfadhili wa safari hizo. Asilimia 8.97 ya watahiniwa waliochagua C “Cecil Rhodes” na asilimia 6.46 ya watahiniwa waliochagua E “Henry Stanley” walishindwa kutofautisha kati ya mfadhili wa safari za kipelelezi na vitangulizi vya ukoloni.

**Kielelezo Na.2.2.11:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.




**Kielelezo Na.2.2.11** *kinaonesha kuwawatahiniwa wengi walishindwa kuchagua jibu sahihi.*


**Swali la 32:** Soko kuu la watumwa Afrika Mashariki lilikuwa

A Zanzibar
B Mombasa
C Kilwa
D Bagamoyo
E Nairobi.

Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha mji ambamo soko kuu la watumwa Afrika Mashariki lilikuwa. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani ni watahiniwa 269,858 tu sawa na asilimia 35.34 walioweza kuchagua jibu sahihi A “Zanzibar” (angalia Kielelezo Na.2.2.12). Aidha, watahiniwa wengi (61.39%) waliochagua vipotoshi B “Mombasa”, C “ Kilwa” na D “Bagamoyo” walikuwa na uelewa kuhusu masoko ya

watumwa katika Afrika Mashariki lakini walishindwa kubaini lipi lilikuwa ni soko kuu la watumwa. Hata hivyo, asilimia 2.69 ya watahiniwa walichagua kipotoshi E “Nairobi” pengine kwa sababu Nairobi ni “Mji Mkuu” hivyo walidhani hata “soko kuu” lingepatikana kwenye mji huo.

**Kielelezo Na.2.2.12:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika kila Chaguo.




**Kielelezo Na.2.2.12** *kinaonesha kuwa ni watahiniwa wachache tu waliweza kuchagua jibu sahihi*.

## 2.3 sehemu C: Jiografia


**Swali la 33:** Nchi ya Japani ina uwezo wa kufanya biashara kuliko Tanzania kwa sababu ina

A watu wengi zaidi
B eneo kubwa la biashara
C shule nyingi za biashara
D teknolojia ya juu zaidi
E wafanyabiashara wengi zaidi.

Swali hili lillipima maarifa ya watahiniwa kuhusu sababu ya nchi ya Japani kuwa na uwezo wa kufanya zaidi biashara kuliko Tanzania. Mtahiniwa alitarajiwa kubaini kuwa uwezo wa Japani kufanya biashara zaidi kuliko Tanzania unatokana hasa na tofauti katika maendeleo ya teknolojia kati ya nchi hizi mbili. Kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 2.3.1**, swali hili lilijibiwa kwa kiwango cha wastani kwani asilimia 59.39 ya watahiniwa waliweza kuchagua D “teknolojia ya juu zaidi” ambalo ndilo lilikuwa jibu sahihi.

Pamoja na kwamba kipotoshi B “eneo kubwa la biashara” pia kilivutia asilimia 17.62 ya watahiniwa hakielezi kwa kutosheleza sababu za Japani kuwa na uwezo wa kufanya biashara zaidi kuliko Tanzania. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika vipotoshi A, B, C na E unaonesha ufinyu wa maarifa ya watahiniwa katika kujibu swali hili.

**Kielelezo Na. 2.3.1:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo.




***Kielelezo Na. 2.3.1**: kinaonesha ufaulu wa wastani ambapo asilimia 59.39 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.*

**Swali la 34:** Mchoro mkato wa ramani huonesha

A mazao na mazingira

B sura ya nchi

C mazingira ya eneo husika


D hali ya hewa

E makazi ya watu na shughuli za kiuchumi.

Katika swali hili, watahiniwa walitakiwa kubainisha kitu ambacho mchoro mkato wa ramani huonesha. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa kama zilivyoainishwa katika **Kielelezo Na. 2.3.2** zinaonesha kuwa asilimia 48.82 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi B “sura ya nchi”. Jibu hili lilikuwa sahihi kwa kuwa mistari ya kontua pamoja na michoro mkato itokanayo na kontua hizo huonesha sura ya nchi na siyo

taarifa zingine za kijiografia. Kwa mantiki hiyo, pamoja na kwamba vipotoshi A, C, D na E vinawakilisha taarifa ambazo zinaweza kuoneshwa kwenye ramani, siyo majibu sahihi. Kwa watahiniwa kuchagua vipotoshi A, C, D na E ni kilelezo cha stadi hafifu za usomaji ramani walizonazo watahiniwa hao.

**Kielelezo 2.3.2:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo.





***Kielelezo Na. 2.3.2:*** *kinaonesha ufaulu wa wastani ambapo asilimia48.82 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.*

**Swali la 35:** Mlima mrefu kuliko yote barani Africa ni

A Drakensburg
B Everesti
C Atlasi
D Kenya
E Kilimanjaro.

Swali lilipima maarifa ya watahiniwa kuhusu sura ya nchi ya Bara la Afrika hususan mlima mrefu kuliko yote. Kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 2.3.3**, asilimia 66.65 ya watahiniwa waliofanya mtihani waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni E "Kilimanjaro". Ufaulu huu unaweza kuwa umetokana na ukweli kwamba, mlima Kilimanjaro unapatikana nchini Tanzania na watahiniwa hupata taarifa zake kwa namna tofauti tofauti kama vile matangazo ya vivutio vya utalii kwenye vyombo vya habari. Aidha, asilimia 10.88 ya watahiniwa walijibu kwa kuchagua vipotoshi kati ya A, C, na D ambavyo sio majibu sahihi ingawa ni milima inayopatikana barani Afrika. Aidha, asilimia 22.08 ya watahiniwa walichagua kipotoshi B "Everesti". Pamoja na ukweli kwamba mlima Everesti ndiyo mlima mrefu kuliko yote duniani, mlima huo haupo barani Afrika bali unapatikana barani Asia.

**Kielelezo 2.3.3:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo.




***Kielelezo Na. 2.3.3:*** *kinaonesha ufaulu mzuri ambapo asilimia 66.65 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.*

**Swali la 36:** Moja kati ya zifuatazo ni sifa ya picha

A kimo halisi huonekana

B sehemu zake zote huonekana

C umbo linaweza kupunguzwa au kuongezwa

D rangi halisi ya kitu haionekani

E rangi ya picha haiwezi kubadilishwa.

**Jedwali Na. 2.3.1:** Idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 108,335 | 135,785 | 359,016 | 54,269 | 102,227 | 3,903 |
| Asilimia ya watahiniwa | 14.19 | 17.78 | 47.02 | 7.11 | 13.39 | 0.51 |

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kuchambua sifa za picha. Kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2.3.1**, ufaulu katika swali hili ni wa kiwango cha wastani kwani watahiniwa 359,016 sawa na asilimia 47.02 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walichagua jibu sahihi ambalo ni C “umbo linaweza kupunguzwa au kuongezwa”. Kwa upande mwingine, asilimia 52.47 ya watahiniwa waliochagua vipotoshi A, B, D na E hawakuweza kuchambua kwa makini na hivyo kushindwa kubaini udhaifu uliokuwa kwenye vipotoshi hivyo hali iliyofanya wachague majibu yasiyo sahihi. Hali hii inaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo katika mada hii.

**Swali la 37:** Kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari kutokana na kuyeyuka kwa barafu katika ncha za kaskazini na kusini kunaweza kusababisha

A Wavuvi kuzama baharini

B Uharibifu wa maeneo ya pwani

C Upungufu wa samaki

D Mvua za el-nino

E Kutokea kwa tsunami

**Jedwali Na. 2.3.2:** Idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 121,958 | 215,428 | 140,678 | 123,812 | 154,992 | 6,667 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 15.97 | 28.21 | 18.42 | 16.22 | 20.3 | 0.87 |

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini athari zitokanazo na kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari kutokana na kuyeyuka kwa barafu katika ncha za Kaskazini na Kusini. Ufaulu katika swali hili kama unavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 2.3.2** haukuwa wa kuridhisha kwani watahiniwa 541,440 sawa na asilimia 70.91 walichagua vipotoshi A, C, D na E. Ni watahiniwa 215,428 tu sawa na asilimia 28.21 ndio walichagua B “uharibifu wa maeneo ya pwani” ambalo lilikuwa jibu sahihi. Uchaguzi wa watahiniwa katika vipotoshi A, C, D na E unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uhusiano uliopo kati ya kuyeyuka kwa barafu katika ncha za kaskazini na kusini na athari zake katika mazingira ya pwani. Aidha watahiniwa asilimia 20 waliochagua E “Kutokea kwa tsunami”

ni kielelezo kuwa hawakuwa na ufahamu wa jinsi tsunami inavyotokea.

**Swali la 38:** Ikiwa ni saa 12:00 jioni Tanzania ambayo ipo nyuzi 45 mashariki, itakuwa saa ngapi Rwanda ambayo ipo nyuzi 30 mashariki?

A 1:00 Usiku.

B 2:00 Usiku.

C 11:00 Jioni.

D 12:00 Jioni.

E 10:00 Jioni.

**Jedwali Na. 2.3.3:** Idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 144,833 | 153,018 | 324,396 | 64,959 | 70,438 | 5,891 |
| Asilimia ya watahiniwa | 18.97 | 20.04 | 42.49 | 8.51 | 9.23 | 0.77 |

Swali hili lilipima stadi za watahiniwa katika kutumia mistari ya longitudo katika kukokotoa muda. Katika kujibu swali hili kwa ufasaha ujuzi wa kanda za muda ungeweza kusaidia katika kubaini jibu sahihi kwa urahisi zaidi. Takwimu katika **Jedwali Na. 2.3.3** zinaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa wa kiwango cha wastani. Jumla ya watahiniwa 324,396 sawa na asilimia 42.49 walichagua C “11:00 Jioni”. Jibu hili ni sahihi kwa kuwa Tanzania ambayo ipo katika nyuzi 45º mashariki itakuwa mbele saa moja zaidi ya Rwanda ambayo iko katika nyuzi 30º mashariki. Kwa sababu hiyo asilimia 56.73 ya watahiniwa waliochagua vipotoshi A, B, D na E hawakuwa na

maarifa ya kutosha ya matumizi ya longitudo katika kukokotoa muda wala uelewa wa kutosha wa kanda za muda hali iliyowafanya washindwe kukokotoa au kubaini jibu sahihi.

**Swali la 39:** Madhara gani kati ya yafuatayo yanatokana na mlipuko wa volkeno?

A Kuharibika kwa miundombinu.

B Kupungua kwa eneo la kilimo.


C Ongezeko la maradhi ya ngozi.

D Ongezeko la mvua za El-nino.

E Kuongezeka kwa ukame.

Katika swali hili watahiniwa walitarajiwa kuonesha uelewa wa madhara yatokanayo na mlipuko wa volkeno. Ufaulu katika swali hili kama unavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 2.3.4** unaonesha kuwa asilimia 33.58 ya watahiniwa walichagua A “kuharibika kwa miundombinu”. Asilimia ya watahiniwa waliobakia (37.77%) walichagua vipotoshi ambayo havina uhusiano wa moja kwa moja na mlipuko wa volkeno. Kati ya watahiniwa hao, asilimia 24.51 walivutiwa na kipotoshi E “kuongezeka kwa ukame”. Watahiniwa hao hawakuweza kubaini kuwa mlipuko wa volkeno hauna uhusiano wa moja kwa moja na mabadiliko ya hali ya hewa yanayosababisha kuongezeka kwa ukame.

**Kielelezo 2.3.4:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo.




***Kielelezo Na. 2.3.4:*** *kinaonesha ufaulu hafifu ambapo asilimia 33.58 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.*

**Swali la 40:** Nchi ipi ni maarufu kwa uundaji wa meli duniani?

A Urusi.

B Uingereza.

C Japani.


D Ufaransa.

E Canada.

Swali hili lilipima maarifa ya watahiniwa kubaini nchi ambayo ni maarufu katika utengenezaji wa meli duniani. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kama unavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 2.3.5** ni mzuri kwani, asilimia 63.32 ya watahiniwa walichagua C “Japani” ambalo lilikuwa jibu sahihi. Watahiniwa waliobaki (36.07%) walichagua vipotoshi A ‘’urusi” (12.6%), B “uingereza” (9.27%), D “Ufaransa” (5.77%) na E “Canada” (24.51%) kwani watahiniwa hawa hawakuwa

na maarifa ya kutosha kuhusu nchi mbalimbali na vitu ambavyo nchi hizo ni maarufu katika uundaji.

**Kielelezo 2.3.5:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo




***Kielelezo Na. 2.3.5:*** *kinaonesha ufaulu mzuri ambapo asilimia 63.32 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.*

**Swali la 41:** Uelekeo wa sehemu katika ramani hubainishwa kwa kutumia

A Dira
B Fremu
C Skeli
D Ufunguo
E Jina la ramani.

**Jedwali Na. 2.3.4:** Idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 506,900 | 41,620 | 51,635 | 121,178 | 37,538 | 4,664 |
| Asilimia ya watahiniwa | 66.39 | 5.45 | 6.76 | 15.87 | 4.92 | 0.62 |

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kutambua matumizi ya mambo muhimu katika ramani. Hili ni kati ya maswali ambayo watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri. Kama inavooneshwa kenye **Jedwali Na. 2.3.4**, watahiniwa 506,900 sawa na asilimia 66.39 walichagua A “Dira” ambalo ndilo jibu sahihi. Kwa upande mwingine, watahiniwa 214,971 sawa na asilimia 32.98 walichagua vipotoshi B, C, D na E. Pamoja na ukweli kwamba vipotoshi hivi vyote vilihusu mambo muhimu katika ramani, mtahiniwa alitakiwa kuonesha bayana alama inayotumika katika kuonesha uelekeo ambayo ni Dira. Kati ya watahiniwa hao, watahiniwa 121,178 sawa na asilimia 15.87 walivutika na kipotoshi D “Ufunguo”. Uchaguzi huu unaweza kuwa umesababishwa na ukweli kuwa watahiniwa walichanganya dhana hizi mbili.

**Swali la 42:** Bahari ya Hindi ipo upande gani wa Tanzania?

A Kusini.

B Kaskazini.

C Magharibi.

D Mashariki.

E Kusini magharibi.

**Jedwali na. 2.3.5:** Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika Kila Chaguo.

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 74,342 | 92,561 | 116,725 | 422,070 | 53,285 | 4,552 |
| Asilimia ya watahiniwa | 9.74 | 12.12 | 15.29 | 55.28 | 6.98 | 0.60 |

Katika kujibu swali hili, watahiniwa walitakiwa kuwa na uelewa wa mipaka ya nchi ya Tanzania pande zote. Watahiniwa pia walitakiwa kuwa na uwezo wa kutumia stadi sahili za ramani ambazo zingewawezesha kutambua ni upande gani wa Tanzania umepakana na Bahari ya Hindi. Kama **Jedwali Na. 2.3.5** linavyoonesha, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 422,070 sawa na asilimia 55.28 walichagua jibu sahihi ambalo ni D "mashariki". Kwa upande mwingine, asilimia 44.13 ya watahiniwa waliochagua vipotoshi A, B, C na E walionesha kuwa na uelewa mdogo wa mipaka ya nchi ya Tanzania pamoja na vitu inavyopakana navyo kama vile bahari.

**Swali la 43:** Uoto unaoathiri mazingira ya ziwa Victoria ni

A nyasi ndefu

B vichaka

C mikoko

D miiba

E magugu maji.

**Jedwali Na. 2.3.6:** Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika Kila Chaguo.

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 97,815 | 95,531 | 134,440 | 55,522 | 373,783 | 5,444 |
| Asilimia ya watahiniwa | 12.81 | 12.51 | 17.61 | 7.27 | 49.09 | 0.71 |

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini aina ya uoto unaoathiri mazingira ya ziwa Victoria. Uchambuzi katika swali

hili kama unavyooneshwa kenye **Jedwali Na. 2.3.6** unaonesha ufaulu wa wastani. Jumla ya watahininiwa 373,783 sawa na asilimia 49.09 ya watahiniwa wote waliweza kuchagua E “magugu maji” ambalo lilikuwa jibu sahihi. Hata hivyo, asilimia 17.61 ya watahiniwa walichagua C “mikoko”. Pamoja na kwamba mikoko ni uoto unaoota kando kando ya mazingira ya maji, uoto huo hupatikana kando kando ya bahari na siyo ziwani. Kwa upande mwingine, asilimia 12.81 na 12.51 ya watahiniwa walichagua A na B kwa mfuatano mtawalia ambayo hayakuwa majibu sahihi. Watahiniwa hawa walionesha kuchanganya uoto huu, ambayo ni dalili ya kutokuwa na maarifa ya kutosha yanayowafanya wasiwe na uhakika na majibu yao.


**Swali la 44:** Uoto unaopatikana katika eneo la Ikweta ni

A uoto wa savana
B vichaka vyenye nyasi ndefu
C misitu minene
D misitu minene na nyasi fupi
E vichaka na nyasi fupi.

Katika swali la 44 watahiniwa walitakiwa kubainisha uoto unaopatikana katika eneo la Ikweta. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili kama unavyoonehswa kwenye **Kielelezo Na. 2.3.6** haukuwa wa kuridhisha. Asilimia 35.65 tu ya watahiniwa waliofanya mtihani waliweza kuchagua C “misitu minene” ambalo lilikuwa jibu sahihi. Kipotoshi A “uoto wa savana” kilivutia watahiniwa 194,221 sawa na asilimia 25.44. Uchaguzi huo unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa wa

kutosha wa eneo la Ikweta na sifa zake. Aidha, majibu ya watahiniwa waliofanya chaguo B “vichaka vyenye nyasi ndefu” (12.01%), D “misitu minene na nyasi fupi” (19.73%) na E “vichaka na nyasi fupi” (19.73%) yalitofautiana ambayo ni dalili ya ufinyu wa uelewa katika mada hii.

**Kielelezo Na. 2.3.6:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo.




***Kielelezo Na. 2.3.6:*** *kinaonesha ufaulu hafifu ambapo asilimia 35.65 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.*


**Swali la 45:** Ziwa lenye kina kirefu zaidi Afrika ya Mashariki ni

A Natron
B Turkana
C Viktoria
D Tanganyika
E Nyasa.

Swali hili lililenga kupima uwezo wa watahiniwa katika kutambua kina cha maziwa yaliyopo Afrika Mashariki. Kama takwimu zinavyoonesha katika **Kielelezo Na. 2.3.7**, hili ni moja kati ya maswali yenye ufaulu wa wastani. Takwimu

zinaonesha kuwa, asilimia 55.9 walijibu swali hili kwa usahihi kwa kuchagua chaguo D “Tanganyika”. Aidha, asilimia 22.15 walichagua kipotoshi C “Viktoria”. Sababu za watahiniwa wengi kiasi hiki kuchagua kipotoshi hicho zinaweza kuwa zinatokana na ukweli kuwa ziwa Viktoria ni kubwa kuliko maziwa yote ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, huenda walihusisha ukubwa wa ziwa na urefu wa kina chake. Aidha watahiniwa waliochagua A “Natroni” (5.85%), B “Turkana” (9.1%) na E “Nyasa” (6.42%) inaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na ufahamu finyu wa mada husika.

**Kielelezo Na. 2.3.7:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo




***Kielelezo Na. 2.3.7:*** *kinaonesha ufaulu wa wastani ambapo asilimia 55.9 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.*

**Swali la 46:** Kitu muhimu katika ramani kinachotumika kuonesha uwiano wa umbali katika ramani na umbali halisi kwenye ardhi huitwa

A Kipimio
B Dira
C Ufunguo
D Fremu
E Jina la ramani.

**Jedwali Na. 2.3.7** Idadi na Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa katika Kila Chaguo.

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 471,578 | 108,115 | 94,435 | 61,450 | 23,468 | 4,489 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 61.76 | 14.16 | 12.37 | 8.05 | 3.07 | 0.59 |

Katika swali hili, watahiniwa walitakiwa kubaini kitu muhimu katika ramani kinachotumika kuonesha uwiano wa umbali katika ramani na umbali halisi kwenye ardhi. Uchambuzi katika swali hili unaonesha kuwa ufaulu ulikuwa mzuri. Kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 2.3.7**, asilimia 61.76 ya watahiniwa walichagua A "Kipimio" ambalo lilikuwa ni jibu sahihi. Aidha, watahiniwa waliochagua vipotoshi B, C, D, na E wameonesha kutokuwa na maarifa ya kutosha hasa kuhusu kazi ya vitu muhimu katika ramani na hivyo kusababisha wachague majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano chaguo B "Dira" ambalo lilichaguliwa na asilimia 14.16 ya watahiniwa hutumika kuonesha upande wa kaskazini mwa ramani, na C "Ufunguo" lililochaguliwa na asilimia 12.37 ya watahiniwa hutumika kuonesha maana ya alama mbalimbali zilizotumika

katika ramani, D “Fremu” (8.05%) hutumika kuonesha mwisho wa ramani na E “Jina la ramani” (3.07%) kuonesha sehemu na madhumuni ya ramani hiyo.

**Swali la 47:** Nishati gani kati ya zifuatazo inaweza kusababisha uharibifu wa mazingira?

A Jua.

B Upepo.


C Maji.

D Mkaa.

E Kinyesi cha wanyama.

Swali la 47 lilikuwa linawapima watahiniwa uwezo wao wa kubaini nishati ambayo inaweza kusababisha uharibifu wa mazingira. Uchambuzi katika swali hili unaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani. Kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 2.3.8**, asilimia 41.66 tu waliojibu swali kwa usahihi kwa kuchagua D “Mkaa”. Majibu ya watahiniwa wengine waliobakia yalikuwa na mtawanyiko katika vipotoshi hali iliyoonesha kuwa hawakuwa na uhakika wa jibu sahihi. Watahiniwa waliochagua A “Jua” (9.38%), B “Upepo” (20.05%), C “Maji” (7.96%) na E “Kinyesi cha wanyama” (20.35%) walishindwa kuelewa kuwa nishati hizo zote ni rafiki kwa mazingira hivyo haziwezi kusababisha uharibifu wa mazingira.

**Kielelezo Na. 2.3.8:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo.




***Kielelezo Na. 2.3.8:*** *kinaonesha ufaulu wa wastani ambapo asilimia 41.66 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.*

**Swali la 48:** Ufugaji wa kisasa wa wanyama huzingatia nini?

A Utamaduni wa jamii.

B Ubora wa wanyama na mazao yao.

C Kuwapo kwa ardhi ya kutosha.


D Mbuga za asili za kulishia mifugo.

E Hali ya hewa.

Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kutambua mambo ya kuzingatia katika ufugaji wa kisasa wa wanyama. Uchambuzi unaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ni hafifu. Kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 2.3.9**, asilimia 38.9 tu ya watahiniwa waliofanya mtihani walichagua jibu sahihi ambalo ni B “Ubora wa wanyama na mazao yao”. Watahiniwa waliochagua vipotoshi A “Utamaduni wa jamii” (6.42%), C “Kuwapo kwa ardhi ya kutosha” (23.24%) na D “Mbuga za asili za kulishia mifugo” (17.55%) walishindwa kutofautisha

kati ya mahitaji muhimu katika ufugaji wa asili wa wanyama na mahitaji muhimu katika ufugaji wa kisasa.

**Kielelezo Na. 2.3.9:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo.




***Kielelezo Na. 2.3.9:*** *kinaonesha ufaulu hafifu ambapo asilimia 38.9 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.*


**Swali la 49:** Majira ya mwaka hutokea kutokana na

A kupatwa kwa mwezi
B mwezi kuizunguka dunia
C dunia kulizunguka jua
D kupatwa kwa jua
E kuongezeka kwa joto.

Katika kujibu swali hili watahiniwa walitakiwa kubaini kitu kinachosababisha kutokea kwa majira ya mwaka. Kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 2.3.10**, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri. Uchambuzi unaonesha kuwa, asilimia 64.64 ya watahiniwa walichagua C "dunia kulizunguka jua"

ambalo ni jibu sahihi. Aidha, watahiniwa waliochagua vipotoshi A “kupatwa kwa mwezi” (11.94%), B “mwezi kuizunguka dunia” (10.36%), D “kupatwa kwa jua” (8.51%) na E “kuongezeka kwa joto” (4.05%) wanaonekana kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mfumo wa jua na hasa mizunguko mbalimbali ya sayari dunia na athari zake kitu kinachoonesha uelewa mdogo katika mada hii.

**Kielelezo Na. 2.3.10:** Asilimia ya Majibu ya Watahiniwa Katika Kila Chaguo.




***Kielelezo Na. 2.3.10:** kinaonesha ufaulu mzuri ambapo asilimia 64.64 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.*

**Swali la 50:** Mikoa ipi ina mashamba makubwa ya Chai?

A Pwani na Iringa.

B Ruvuma na Morogoro.

C Morogoro na Iringa.

D Kilimanjaro na Mbeya.

E Mbeya na Iringa.

**Jedwali Na. 2.3.8:** Idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 104,648 | 96,101 | 141,474 | 151,606 | 265,630 | 4,076 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.71 | 12.59 | 18.53 | 19.86 | 34.79 | 0.53 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kubaini mikoa ambayo ina mashamba makubwa ya Chai. Uchambuzi uanonesha kuwa, watahiniwa wengi walikuwa na uelewa hafifu katika swali hili. Kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 2.3.8**, asilimia 34.79% ya watahiniwa walichagua E “Mbeya na Iringa” ambalo lilikuwa jibu sahihi. Aidha, majibu ya watahiniwa waliochagua vipotoshi A, B, C na D yalikuwa na mtawanyiko uliioonesha kuwa walikuwa na uelewa finyu juu ya mada husika.

## 3.0 UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI

Uchambuzi wa mada zilizofanyika kwa vibaya (uhafifu), wastani na vizuri umefanyika. Mada zilizofayika vibaya (hafifu) zilikuwa na wastani wa ufaulu kati ya 0 – 40 (nyekundu), wastani 41 – 60 (njano) na nzuri 61 – 100 (kijani).

Baadhi ya mada zilikuwa na ufaulu mzuri ilhali mada zingine zilikuwa na ufaulu wa wastani na zingine ufaulu hafifu. Mada zilizokuwa na ufaulu mzuri ni Alama za Taifa, Utamaduni wa Tanzania na Tamaduni nyingine, Ushirikiano kati ya Tanzania na mataifa mengine, Familia Yetu na Mawasiliano na biashara. Watahiniwa wengi walionesha uwezo wa kuelewa

mada kwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo walivyopewa.

Mada zingine kama vile Uongozi katika Ngazi ya Familia na Shule, Demokrasia, Ulinzi na Usalama katika Shule/Taifa, Misingi ya Demokrasia Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar, Vitangulizi vya Ukoloni, Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika Kuanzia mwaka 1880, Jitihada za Kupigania Uhuru katika Afrika, Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru, Usomaji wa ramani, Picha, Mfumo wa Jua na Mazingira zilikuwa na ufaulu wa wastani.

Mada zilizokuwa na ufaulu hafifu ni pamoja na Serikali za Mitaa, Uchumi Wetu, Hatua za Maendeleo Katika Zama Mbalimbali, Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiafrika, Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiasia na Kizungu, Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Afrika, Ushirikiano wa Kimataifa na Shughuli za Kiuchumi. **Viambatisho A** na **B** vinaonesha mchanganuo wa ufaulu katika kila mada. Kwa ujumla, ufaulu wa mada 12 katika somo la Maarifa ya Jamii kwa mwaka 2015 umeongezeka ukilinganishwa na mwaka 2014. Aidha, ufaulu katika mada 9 umeshuka.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa wengi waliweza kuchagua jibu sahihi katika baadhi ya maswali jambo linaloonesha kuwa walikuwa na

maarifa na ujuzi wa kutosha katika mada husika. Aidha, yapo pia maswali ambayo watahiniwa hawakuweza kuchagua majibu sahihi jambo linaloashiria kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika au hawakuelewa matakwa ya swali.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha elimu na ufaulu kwa ujumla Baraza la Mitihani linashauri yafuatayo:

(a) Walimu waweke mkazo katika kufundisha mada zote hususan mada ambazo watahiniwa hawakufanya vizuri katika mtihani wa mwaka huu zitiliwe msisitizo kama ilivyoainishwa katika taarifa hii ya uchambuzi.

(b) Watahiniwa waelimishwe namna ya kusoma maswali kwa umakini ili waweze kubaini matakwa ya kila swali kabla ya kuharakisha.

(c) Watahiniwa wahimizwe kusoma vitabu vingi tena vya kiada na ziada ili waweze kujiongezea maarifa yatakayowawezesha kujibu mitihani vizuri.

(d) Walimu watunge maswali ya majaribio na mitihani ya mihula ambayo yatawapa ujuzi watahiniwa katika kujibu maswali yanayohitaji umahiri.

(e) Mamlaka zinazohusika zifuatilie ufundishaji na ujifunzaji wa watahiniwa katika somo hili ili kuweza kubaini changamoto mbalimbali na kuzipatia majibu ili kuweza kuboresha kiwango cha ufaulu.

*Kiambatanisho A*

## UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA KATIKA PSLE 2015 IKILINGANISHWA NA PSLE 2014

| Na. | Mada | Mtihani wa 2014 | | | | Mtihani wa 2015 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | Asilimia ya ufaulu | | | Namba ya swali | Asilimia ya ufaulu | | |
| 1 | Uongozi katika ngazi ya Familia na Shule | 1 | 43.80 | 43.8 | Wastani | 1 | 58.36 | 58.36 | Wastani |
| 2 | Serikali za Mitaa | 2 | 62.20 | 38.22 | Hafifu | 2 | 35.02 | 36.06 | Hafifu |
| | | 3 | 14.23 | | | 3 | 37.11 | | |
| 3 | Demokrasia | 6 | 57.60 | 53.23 | Wastani | 6 | 47.85 | 44.61 | Wastani |
| | | 7 | 62.10 | | | 7 | 58.72 | | |
| | | 8 | 40.00 | | | 8 | 27.28 | | |
| 4 | Alama za Taifa | 4 | 77.73 | 47.07 | Wastani | 4 | 73.99 | 63.91 | Vizuri |
| | | 5 | 16.4 | | | 5 | 53.83 | | |
| 5 | Ulinzi na Usalama katika Shule/Taifa | 9 | 60.5 | 67.25 | Vizuri | 9 | 47.71 | 44.99 | Wastani |
| | | 10 | 74 | | | 10 | 42.28 | | |
| 6 | Utamaduni wa Tanzania na Tamaduni nyingine | 11 | 10.63 | 10.63 | Hafifu | 13 | 64.37 | 64.37 | Vizuri |
| 7 | Uchumi Wetu | 12 | 52.8 | 52.8 | Wastani | 12 | 14.98 | 14.98 | Hafifu |
| 8 | Ushirikiano kati ya Tanzania na Mataifa mengine | 13 | 26.36 | 26.36 | Hafifu | 13 | 64.37 | 64.37 | Vizuri |
| 9 | Misingi ya Demokrasia | 14 | 57.14 | 57.14 | Wastani | 14 | 52.6 | 52.63 | Wastani |
| 10 | Familia Yetu | 25 | 69.22 | 69.22 | Vizuri | 15 | 90.59 | 88.4 | Vizuri |
| | | | | | | 16 | 86.24 | | |
| 11 | *Ukoo Wetu | 16 | 56.65 | 56.65 | Wastani | - | - | - | - |
| 12 | *Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu | 20 | 8.33 | 22.5 | Hafifu | - | - | - | - |
| | | 32 | 36.66 | | | | | | |
| 13 | Hatua za Maendeleo ya Binadamu Katika Zama | 19 | 51.61 | 51.61 | Wastani | 17 | 44.1 | 32.89 | Hafifu |
| | | | | | | 18 | 21.68 | | |


| Na. | Mada | Mtihani wa 2014 | | | | Mtihani wa 2015 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | Asilimia ya ufaulu | | | Namba ya swali | Asilimia ya ufaulu | | |
| | Mbalimbali | | | | | | | | |
| 14 | *Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiafrika | - | | - | - | 20<br>28 | 45.46<br>32.93 | 39.2 | Hafifu |
| 15 | Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiasia na Kizungu | 15<br>28<br>29 | 15.09<br>22.54<br>21.99 | 19.87 | Hafifu | 19<br>31<br>32 | 46.6<br>16.18<br>35.34 | 33.71 | Hafifu |
| 16 | Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Afrika | 27 | 57.04 | 57.04 | Wastani | 22 | 26.08 | 26.08 | Hafifu |
| 17 | Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar | 24 | 19.67 | 19.67 | Hafifu | 21<br>29 | 52.62<br>60.27 | 56.45 | Wastani |
| 18 | Vitangulizi vya Ukoloni | 23 | 46.69 | 46.69 | Wastani | 30 | 43.7 | 43.7 | Wastani |
| 19 | Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika Kuanzia Mwaka 1880 | 17<br>26<br>30 | 65.64<br>32.86<br>18.91 | 39.14 | Hafifu | 23 | 52.5 | 52.5 | Wastani |
| 20 | Jitihada za Kupigania Uhuru katika Afrika | 21<br>31 | 24.63<br>47.37 | 36 | Hafifu | 26 | 42.27 | 42.27 | Wastani |
| 21 | Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru | 18<br>22 | 36.62<br>42.57 | 39.6 | Hafifu | 24<br>25 | 65.44<br>27.22 | 46.33 | Wastani |
| 22 | *Ushirikiano wa Kimataifa | - | - | - | - | 27 | 38.15 | 38.15 | Hafifu |
| 23 | *Maji | 36 | 67.73 | 67.73 | Nzuri | - | - | - | - |
| 24 | Mazingira | 34<br>35 | 78.7<br>47.7 | 49.39 | Wastani | 35<br>39 | 66.7<br>33.6 | | |

| Na. | Mada | Mtihani wa 2014 | | | | Mtihani wa 2015 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | Asilimia ya ufaulu | | | Namba ya swali | Asilimia ya ufaulu | | |
| | | 39 | 49.99 | | | 43 | 49.1 | 47.12 | Wastani |
| | | 42 | 80.88 | | | 44 | 35.7 | | |
| | | 44 | 41.58 | | | 45 | 55.9 | | |
| | | 47 | 26.87 | | | 47 | 41.7 | | |
| | | 41 | 48.57 | | | | | | |
| | | 48 | 42.5 | | | | | | |
| | | 49 | 42.4 | | | | | | |
| 25 | Picha | 38 | 50.43 | 50.43 | Wastani | 36 | 47 | 47 | wastani |
| 26 | Mfumo wa Jua | 33 | 34 | 30.21 | Hafifu | 38 | 42.5 | 53.55 | Wastani |
| | | 43 | 26.42 | | | 49 | 64.6 | | |
| 27 | Usomaji wa ramani | 37 | 18.93 | 34.83 | Hafifu | 34 | 48.82 | 58.08 | Wastani |
| | | 40 | 48.58 | | | 41 | 66.4 | | |
| | | 45 | 62.21 | | | 42 | 55.3 | | |
| | | 50 | 9.62 | | | 46 | 61.8 | | |
| 28 | *Majanga | 46 | 34.03 | 34.03 | Hafifu | - | - | - | - |
| 29 | Mawasiliano, Biashara na Uchukuzi | | | | | 40 | 63.3 | 63.3 | Mzuri |
| 30 | *Shughuli za kiuchumi | - | - | - | - | 37 | 28.7 | 34.13 | Hafifu |
| | | | | | | 48 | 38.9 | | |
| | | | | | | 50 | 34.8 | | |


*Kiambatisho B*

## UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA KATIKA PSLE 2015 IKILINGANISHWA NA PSLE 2014

### A: URAIA




## B: HISTORIA



Wastani wa Ufaulu (%)
100
90
80
70
60
50
40
30
20
10
0
22.50
51.61
32.89
39.20
19.87
33.71
57.04
26.08
19.67
56.45
46.69
43.70
39.14
52.50
36.00
42.27
39.60
46.33
38.15
Mwanzo wa Ufaulu
Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu
Hatua za Maendeleo ya Binadamu Katika Zama Mbalimbali
Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiafrika
Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiasia na Kizungu
Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Afrika
Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar
Vitangulizi vya Ukoloni
Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika Kuanzia Mwaka 1880
Jitihada za Kupigania Uhuru katika Afrika
Mabadiliko ya Kijamii,Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru
Ushirikiano wa Kimataifa
Mada
Mwaka 2014
Mwaka 2015

## C: JIOGRAFIA



Wastani wa Ufaulu (%)
100
90
80
70
60
50
40
30
20
10
0
49.39
47.12
50.43
47.00
30.21
53.55
34.83
58.08
34.03
61.30
34.13
Mazingira
Picha
Mfumo wa Jua
Usomaji wa ramani
Majanga
Mawasiliano, Biashara na Uchukuzi
Shughuli za kiuchumi
Mada
Mwanzo wa Ufaulu
Mwaka 2014
Mwaka 2015